**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**
*(Barua zote zipitishwe kwa mkurugenzi mtendaji).*

KUMB Na NGOR/DD/SS/F5J/04, 28/03/2022

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi,

.........................................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO 2022/2023 KWA SHULE YA SEKONDARI DIGODIGO**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao ......................................................................... amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO 2022/2023 katika shule ya sekondari Digodigo kwa tahasusi ya EGM/HGK.

**MAHALI SHULE ILIPO:**

1.0 Shule ipo mkoa wa Arusha, wilaya ya Ngorongoro,Kata ya kirangi. Kwa wanaotokea nje ya Wilaya ya Ngorongoro, utapandia Basi/Gari kituo cha mabasi Arusha yaendayo Loliondo (LOLIONDO STATION) na utashukia kituo cha mabasi katika mji mdogo Digodigo. Ukifika mji mdogo wa Digodigo unaweza kufika shule kwa kupanda pikipiki ama ukatembea kwa miguu maana Shule ipo jirani.

2.0 Mwanafunzi amechaguliwa kujiunga na Tahasusi/mchepuo wa EGM/HGK
Shule itafunguliwa tarehe ................................ siku ya jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 10:00 jioni siku hiyo hiyo ya jumamosi.

3.0 **Sare ya shule na mavazi mengine ya kushindia shuleni.**

i. Shati mbili (2) nyeupe za mikono mirefu zisizobana mwili.
ii. Sketi mbili (2) za rangi ya karoti (sketi yenye mshono wa V kwa mbele) na ziwe ndefu chini ya magoti.
iii. Skafu rangi ya sketi
iv. Sweta nyeusi 01
v. Gauni mbili damu ya mzee iliyokolea kwa ajili ya kushindia (shamba dress ) urefu chini ya magoti na isiyobana mwili.
vi. T- shirt ya shule inapatikana shuleni kwa bei ya Tshs. 14,000/=
vii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visivyokuwa na visigino na urembo vinavyopigwa rangi.
viii. Stockings (Soksi ndefu) nyeupe jozi mbili (2) zisizo na urembo
ix. Track suit moja ya **kijani** na isiyobana mwili.

**NB: Sare zote zilizo orozeshwa hapo juu mwanafunzi anapaswa kuja nazo isipokuwa T-shirt ya shule inayopatikana shuleni kwa bei elekezwa hapo juu.**

**4.0 Mahitaji ya malazi na bweni**

- Godoro lenye upana futi $2^{1}/_{2}$ aina ya Tanform ama super banco pamoja na mto mmoja.
- Chandarua cha duara rangi nyeupe kwa ajili ya kuzuia mbu. .
- Shuka mbili (2) rangi ya Pink
- Sanduku moja la chuma (tranka)
- Taulo/khanga na ndala za kuogea
- Ndoo moja ya kuogea ya lita 10 au zaidi
- Tochi kwa dharura
- Aje na viatu vya kushindia
- Hard broom moja na squeezer moja
- Aje na sabuni za kutosha za kuogea na kufulia, mafuta ya kupaka, mswaki pamoja na dawa ya meno. Pafymu na mafuta yenye harufu kali haziruhusiwi

**NB: Mwanafunzi apewe fedha za kutosha za matumizi**

**5.0 VIFAA VYA KULIA CHAKULA**

i. Sahani moja ya mfupa
ii. Bakuli moja ya mfupa
iii. Kikombe kimoja cha mfupa
iv. Kijiko
v. Thermos kwa ajili ya kutunzia maji ya moto kwa ajili ya chai.

**6.0 VIFAA VYA MICHEZO**

- T – shirt nyeupe ya Tanzania
- Track suit moja rangi ya kijani
- Raba na socks za michezo rangi yoyote

NB: **mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani tofauti na ilivyoelekezwa.**

**7.0 VIFAA VYA DARASANI**

- Begi zuri na lenye kamba ngumu la kubebea madaftari
- Madaftari makubwa (counter books) 7 au zaidi
- Mathematical set, scientific calculator , ruler, graph pad pamoja na Dictionary kubwa (Advanced learners dictionary)
- Vitabu vya kutosha kulingana na Tahasusi mwanafunzi aliyo chaguliwa.
- Ream paper moja A4
- Aje na saa ya mkononi
- Jalada (file cover) mmoja rangi ya kaki

**8.0 MAAGIZO YA FEDHA, ADA NA MICHANGO MINGINE:**

Kwa kuwa mwanao atahitaji huduma mbalimbali awapo hapa shuleni mwanao atapaswa kuchangia michango mbalimbali pamoja na ada kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:

| MAELEZO | | KIASI | MUDA |
|---|---|---|---|
| i. | Ada | 70,000/= kwa mwaka na 35,000/= kwa mhula. | Ada inaweza kulipwa mara mbili kwa mwaka yaani 35,000/= kwa mhula |
| ii. | Ulinzi , ukarani na upishi | 30,000/= | Kwa mwaka |
| iii. | Ukarabati | 20,000/= | Kwa mwaka |
| iv. | Kuboresha taaluma | 30,000/= | Kwa mwaka |
| v. | Picha na Kitambulisho | 5,000/= | Mara moja |
| vi. | Tahadhari | 10,000/= | Kwa mwaka (Hairejeshwi) |
| vii. | Nishati | 14,000/= | Kwa mwaka |
| viii. | Michezo | 3000/= | Mara moja |
| ix. | matibabu na huduma ya kwanza | 6,000/= | Kwa mwaka |

**Fedha zote za shule zitalipwa kwenye akaunti ya shule ya sekondari digodigo kupitia control number zitakazo tolewa na shule.**

Ili kupata control namba ya kulipia ada na michango mingine wasiliana na:

1.Mkuu wa shule kwa namba ya simu **0754088341** AU **0785758063.**

2.Mhasibu wa shule kwa namba ya simu **0769340712.**

**KUMBUKA:**Unatakiwa kuleta pay inslip ya malipo ya fedha za shule.

**MUHIMU.**

a) Atatakiwa apewe kuthibitisha afya yake kwenye hosipitali ya serikali, Fomu imeambatanishwa kwenye barua hii.
b) Shule haitoi chakula maalum kwa wagonjwa (special diet)
c) Utapokelewa iwapo umeyatekeleza maagizo yote yaliyotolewa hapo juu.
d) Simu haziruhusiwi hapa shuleni (ukikamatwa na simu utarudishwa nyumbani).
e) Tafadhali soma kwa makini maelekezo au maagizo hayo na kuyatekeleza kwa umakini.

**Mwisho**, natumia nafasi hii kukukaribisha hapa shuleni Digodigo sekondari na ni matarajio yangu kuwa ufikapo hapa utatumia vyema nafasi hii uliyotunukiwa na taifa.

**Kumbuka** kama hujaripoti shuleni hadi ifikapo tarehe .................utahesabiwa kuwa umeikataa nafasi hii hivyo itachukuliwa na mwanafunzi mwingine

***KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI DIGODIGO.***

.....................

FIDELIS E. BILALY.
MKUU WA SHULE.

MKUU WA SHULE
TAREHE 28/3/2022
DIGODIGO SEKONDARI

Nakala:
Mthibiti Ubora Mkuu wa Shule
Kanda ya kazkazini magharibi,
SL.P. 807,
Arusha.

Afisa Elimu (M) Arusha,
S.L.P. 2032,
Arusha.

Mkurugenze Mtendaji,
Halmashauri ya (w)Ngorongoro ,
SL.P. 01,
Arusha.

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995 aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.

1. RATIBA
   - i. Mwanafunzi anatakiwa kuamka saa 11:30 asubuhi tayari kwa mchakamchaka na kufanya usafi wa maeneo aliyopangiwa kabla ya muda wa kukusanyika (parade). Hivi ni vipindi kama vipindi vya masomo, hivyo kukosa vipindi au kuchelewa vipindi au kazi yoyote bila sababu maalumu ni uhalifu. Utaadhibiwa kwa kosa hilo na usipojirekebisha utasimamishwa shule hadi ujirekebishe. Hivyo basi, inabidi uheshimu kengele zote zinazogongwa shuleni.
   - ii. Mwanafunzi atakayechelewa kuripoti shuleni siku saba baada ya kufungua shule atarudishwa nyumbani kwa muda utakaoamriwa
   - iii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
2. UTII
   - i. Mwnafunzi anapaswa kutii sheria, kanuni, miongozo na watu wote ipasavyo pasipo ubishi wala kusita na manung'uniko yoyote.
   - ii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
   - iii. Kutunza mali ya umma
   - iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
3. MAZINGIRA NA USAFI
   - i. Mwanafunzi haruhusiwi kutupa aina yoyote ya uchafu kwa mfano makaratasi mahali ambapo siyo mahala pake.
   - ii. Mabweni,madarasa na vyoo vifanyiwe usafi asubuhi
   - iii. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya yafuatayo;
     - Wizi
     - Uasherati na ushoga
     - Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, kubeli n.k.
     - Kupigana au kupiga
     - Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
     - Kuwa mjamzito/kupata mimba na /au kutoa mimba
     - Kuolewa
     - Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule.
     - Kukataa adhabu kwa makusudi.
     - Kuwa na simu ya mkononi au line ya simu
     - Kujaribu kujitoa uhai wewe mwenyewe au mtu mwingine kwa namna yoyoye ile.
     - Kunyoa mitindi isiyo faa
     - Kusuka nywele
     - Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
     - Kufuga kucha
     - Kuongeza urembo wa aina yoyote kwenye sare ya shule
     - Kupaka rangi ya kucha, wanja ama kutinda nyusi
     - Kuvaa bangili, hereni. Shanga n.k

4. AMANI YA SHULE
   Mwanafunzi haruhusiwi kuchokoza, kuonea, kudharau,kutukana na kusengenya. Ukiwa na shida peleka shauri lako kwa viongozi husika au kushirikisha wenzako kwenye vikao halali vya shule. Ni marufuku kufanya mikutano ya siri na yenye nia mbaya ya kuvuruga amani ya shule kwani unaweza kufukuzwa.
5. IMANI NA DINI
   i. Kila mwanafunzi atapaswa kushiriki vipindi vyote vya dini na kufuata sheria, kanuni na miongozo ya dini yake wakati wote awapo shuleni.
   ii. Mwanafunzi atapaswa kuheshimu dini na imani ya mwenzake
   iii. Utumiaji wa spika kwenye mihadhara au mahubiri hairuhusiwi shuleni maana itakuwa usumbufu kwa wengine.
   iv. Shughuli zà kidini zisiathiri ratiba za shule
   v. Waalimu/walezi watakaofika shuleni kwaajili ya kufundisha elimu ya dini lazima watambulishwe ofisi ya mkuu wa shule.

**President's office**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.**

## DIGODIGO SECONDARY SCHOOL
## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.

To be completed by the Government Medical Officer in a Government Hospital in respect of all new entrants to Digodigo Secondary School.

Pupil's full name ……………………………………………………………

Age...............................

01. Blood count (red and white)…………………………………………………..
02. Stool examination………………………………………………………………….
03. Urinalysis…………………………………………………………………
04. T.B test ……………………………………
05. Eye test……………………………………
06. Ear's test……………………………………
07. Chest…………………………………………
08. Spleen……………………………………………………………
09. Girls UPT test……………………………………..
10. HP test ……………………………………………………………………
11. Additional information e.g. Physical defects or impairment infection chronic or family shape etc.

    …………………………………………………………………………………………………

    ……………………………………

I certify that the above mentioned pupil is able/unable to pursue his/her further studies.

Signature…………………………..

Designation………………………

Station ……………………………

Date …………………………………..

Official Stamp

**Jengo la utawala, S.LP. 23, LOLIONDO. Simu:+255785758063,+255754088341**